# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

## OFISI YA WAZIRI MKUU

## TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

# MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE ZA SEKONDARI ZA SERIKALI TANZANIA

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA WAZIRI MKUU – TAMISEMI**


**Namba za Simu**

**Mkuu wa Shule: 0768453828**

**Makamu Mkuu wa Shule.0752557952/0767584572**

**Matron/Patron:0764905410/0765091862**

**Shule ya Sekondari Nyakahura**

**S.L.P.193**

**Biharamulo.**


**Tarehe ……..**

**Mzazi/Mlezi wa Mwanafunzi ..................................................…………**
**……………………………………………**
**S.L.P …..................**
**.................................…………………………………**
**……………………………………………**

**YAH: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE YA SEKONDARI NYAKAHURA HALMASHAURI YA BIHARAMULO MKOA KAGERA MWAKA ………….**

**1.** Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na Kidato cha Tano katika Shule hii mwaka ……..... na atasoma tahasusi ya .......... (CBG/ HGE/ HGK/HGL/ HKL /HGFa/HGLi)

Shule ya Sekondari Nyakahura ipo umbali wa Kilometa 75 Magharibi mwa Mji wa Biharamulo **barabara kuu ya Kahama - Ngara** Usafiri wa basi kutoka mjini Biharamulo unapatikana katika kituo cha mabasi cha Biharamulo Nauli ni Shilingi 6,000/-

Muhula wa Masomo unaanza tarehe ……… hivyo mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni tarehe kuanzia tarehe ……….. Mwisho wa kuripoti ni tarehe ………..

## 2. Mambo muhimu ya kuzingatia:-

### 2.1 Sare za Shule

i. Sare ya shule hii ni sketi nyeusi kitambaa kizito mshono wa rinda box kubwa mbele na nyuma inayofika juu ya kisigino au suruali isiyobana kwa wasichana wa kiislamu . suruali nyeusi yenye marinda mawili kila upande na tanapu (siyo modo)kwa Wavulana . ii. Mashati mawili meupe aina ya tomato mikono mirefu iii. Rangi ya Hijab (kijuba) ni nyeupe ifunike kifua cha mwanafunzi pia iwe ndefu kufikia kifundo cha mkono akisimama

iv. Sare ya Michezo ni Truck suti rangi ya bluu au Nyekundu, jezi rangi ya bluu au nyekundu na raba aina yoyote kwa wasichana na jezi rangi ya bluu au nyekundu kwa wavulana na raba aina yoyote.

v. Viatu vya shule ni vyeusi vya kufunga na kamba vyenye visigino vifupi;

vi. Soksi jozi mbili nyeupe kwa wasichana na nyeusi kwa wavulana .

vii. Mkanda mweusi wa ngozi wa kuvalia suruali;

viii. Sweta la kijani jeshi lenye alama ya ”V” shingoni (inapatikana shuleni)

ix. Nguo za kushindia (*shamba dress*) Gauni moja rangi ya damu ya mzee (maruni) kitambaa cha sukarisukari na sketi moja ya damu ya mzee kitambaa kizito na tsheti rangi ya blue yenye kora na nembo ya shule isiyo na maandishi kwa wasichana (wasichana wa kiislamu wanatakiwa kuwa na hijabu mbili/ ushungi rangi ya damu ya mzee.)

Suruali mbili zenye malinda mawili kila upande rangi ya damu ya mzee na zenye tanapu na tsherti ya bluu yenye kola na nembo ya shule isiyo na maandishi kwa wavulana.

x. Tai rangi ya pundamilia nyeusi na nyeupe yenye misitari midogo midogo kitambaa cha tetroni .

xi. Tisheti (T-shirt) 1 ya shule rangi Nyekundu yenye kola na nembo ya shule ( zinapatikana shuleni)

N:B Rangi za sare



Juba la darasani



Juba la kushindia



Shati



Sketi ya darasani



Suruali ya darasani



Sketi ya kushindia



T-shirt ya darasani



T-shirt ya kushindia



Sweta ya shule



Tai



Shuka

**2.2 Mahitaji mengine muhimu ambayo mwanafunzi anapaswa kuja nayo shuleni:-**

i. Madaftari makubwa (counter Q. 3) 7 na madaftari madogo (msomi) 10 ya majaribio ya kila mwezi ii. **Ream** Mbili (2) A4 kwa mwaka;

iii. Vitabu vya masomo ya tahasusi husika .NB Kila mwanafunzi anashauriwa kuja na kitabu kimojawapo katika masomo ya tahasusi anayosoma.
iv. Dissecting Kit kwa wanafunzi wanaosoma Biology;
v. Scientific Calculator function 991 kwa wanaosoma masomo ya sayansi na biashara.
vi. Godoro lenye vipimo vya futi 2½ x6
vii. Mashuka Jozi 2 (rangi ya pink), blanket 1, foronya ya godoro 1, chandarua 1,
viii. Nguo za ndani za kutosha;
ix. Vyombo vya chakula (sahani, bakuli, kijiko na kikombe);
x. Ndoo 2 kubwa (lita 20) zenye mifuniko;Moja kwa matumizi ya shule na Moja kwa matumizi yake binafsi,beseni 1,toilet paper 5 na Tranka na kufuri kwa ajili ya kutunzia vitu vyake.
xi. **Vifaa vya usafi**

a)Tahasusi za **HKL, HGE, HGL,** na **HGLi** ni ndoo 2, kwanja moja, mopa moja, jembe moja, dawa ya chooni Lita 5, na mfagio mgumu ( hard room) moja.

b) Tahasusi za **CBG, HGK ,**na **HGFa** ni ndoo mbili za Lita 20 moja Kwa matumizi yake na nyingine Kwa matumizi yake binafsi, kwanja moja,dawa ya chooni Lita 5, kotama moja, jembe moja, na mfagio laini ( softbroom) moja.

### 2.3 Michango mbalimbali

| Na | Aina ya Mchango | Kiasi |
|---|---|---|
| 1. | Mchango wa Uendeshaji wa Shule | 65 ,000/ = |
| 3. | Tahadhari | 5 ,000/ = |
| 4. | Nembo | 5 ,000/ = |
| 5. | Kitambulisho cha Shule | 5 ,000/ = |
| | **Jumla** | **80 ,000/ =** |

**MICHANGO YOTE ILIPWE KWENYE AKAUNTI YA SHULE NA MWANAFUNZI AJE NA PAYSLIP YA BENKI SHULENI.AKAUNTI YA SHULE NI NMB 31701200096 NYAKAHURA SECONDARY SCHOOL RECURRENT ACCOUNT.**

## 3. Sheria na Kanuni muhimu za Shule

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyo rekebishwa kwa Sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia yenye dhamana ya elimu na Ofisi ya Rais – TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa

elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yanafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni. Mambo hayo ni pamoja na;

### 3.1 Sheria na Kanuni za Shule

i. Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.;
ii. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule;
iii. Kushiriki kikamilifu masomo ya usiku( Preparation);
iv. Kuwahi katika kila shughuli za shule utakazopewa;
v. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo ya kuwepo ndani na nje ya shule ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii;
vi. Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule;
vii. Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa;
viii. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote;
ix. Kutunza mali za shule;
x. Ni marufuku mwanafunzi kumiliki vifaa vyenye ncha kali na dawa bila idhini ya daktari; na
xi. Mwanafunzi haruhusiwi kubadili dini wala kumshawishi mwanafunzi mwenzake kubadili dini wawapo shuleni.

**MUHIMU:**

- **Mwanafunzi hapaswi kuja na simu shuleni kwa namna yoyote ile, na hakuna mtumishi anayeruhusiwa kutunza simu ya mwanafunzi;**

- **Mwanafunzi awapo shuleni atatakiwa kulala kwenye Bweni alilopangiwa na kitanda alichopangiwa. Ni marufuku mwanafunzi kulala kitanda kimoja na mwenzake au kuishi kwenye Bweni ambalo hakupangiwa. Kitanda kimoja kitatumika na mwanafunzi mmoja tu;**

- **Mwanafunzi ataruhusiwa kurudi nyumbani kwa ruhusa na kibali maalum toka kwa Mkuu wa Shule. (Msiba au Ugonjwa**).
- **Kila mwanafunzi anatakiwa kuja na BIMA YA AFYA au kulipia Tsh. 50,400 kwenye akaunti ya shule ili akatiwe BIMA kwa utaratibu wa BIMA ya AFYA ya NHIF, shule haitahusika na gharama za matibabu ya mwanafunzi.**

**3.2 Makosa yatakayosababisha Mwanafunzi kufukuzwa Shule ni pamoja na :**

i. Wizi;
ii. Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro;
iii. Kugoma na kuhamasisha mgomo;
iv. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii kwa ujumla;
v. Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au mtu yeyote yule;
vi. Kunyoa mtindo usiokubalika na shule mfano panki,kipara au mitindo mingine yoyote ambayo haikubariki kwa mwanafunzi.
vii. Kufuga ndevu;
viii. Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya dawa za kulevya;
ix. Uvutaji wa sigara;
x. Uasherati, mahusiano ya jinsi moja, kuoa au kuolewa;
xi. Kupata ujauzito au kutoa mimba;
xii. Kusababisha mimba;
xiii. Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi;
xiv. Kwenda kwenye nyumba za starehe na nyumba za kulala wageni;
xv. Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule;
xvi. Kudharau Bendera ya Taifa;
xvii. Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu; na
xviii. Uharibifu wa mali ya umma kwa makusudi.

**4. Viambatisho na Fomu Muhimu**


i. Fomu ya Uchunguzi wa Afya (Medical Examination Form) ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa Hospitali ya Serikali;
ii. Fomu ya Maelezo Binafsi kuhusu Historia ya Mwanafunzi/Mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai;
iii. Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yanayotolewa na shule; na
iv. Nakala (copy) za vivuli vya vyeti ,cheti Cha kuzaliwa, living certificate na result slip.

**5.** Tafadhali soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

**KARIBU SANA KATIKA SHULE HII**

**Saini ya Mkuu wa Shule**

**Jina la Mkuu wa Shule BRAISON RAPHAEL UHAKULA**



**Mhuri wa Mkuu wa Shule**




**NB: Kwa siku za hivi karibuni kumekuwa na utapeli (wizi kwa njia ya mitandao). Baadhi ya wazazi wamekuwa wakitumiwa ujumbe mfupi au kupigiwa simu na watu wanaojitambulisha kama walimu na kuwafahamisha kuwa mtoto wa mzazi husika ambaye ni mwanafunzi ni mgojwa na yuko mahututi hivyo mzazi atume pesa. TAFADHALI UPATAPO UJUMBE WOWOTE KUHUSU MWANAFUNZI/MTOTO WAKO USITUME CHOCHOTE, NI VEMA UKAWASILIANA NA UONGOZI WA SHULE KUPATA UKWELI WA TAARIFA HUSIKA KWA NAMBA ZIFUATAZO: -**

- **Mkuu wa shule 0768453828**
- **Makamu Mkuu wa Shule 0752557952 /0767584572**
- **Mwandamizi Taaluma 0757123761**
- **Mwandamizi Malezi 0765091862**

**SHULE YA SEKONDARI – NYAKAHURA.**
**FOMU YA KUANDIKISHWA–SHULE**

( Ijazwe kwa herufi kubwa na irejeshwe kwa mkuu wa shule )

1. Jina kamili……………………………..............................………… ……………uzito katika kilogramu(kg).........urefu wa mwanafunzi katika sentimita (cm)...........

   Tarehe ya kuzaliwa…………………. Wilaya………………Mkoa …………………………
   Taifa …………………Dini:RC/Anglican/Lutheran/Muslim/Pentecoste/n.k.................
   Shule ya sekondari uliyomalizia(kidato cha nne) ……………………………
2. Jina la Baba/Mama/Mlezi …………………..…………………
   Anwani yake ……………………………………………
   Kiwango cha elimu( mf msingi, sekondari, chuo).......…….........................
   Kazi ya Baba /Mama/Mlezi……………………….………………………………
   Namba ya simu…………………………………………………

**AHADI YA MWANAFUNZI.**

(a) Mimi………………………………………..nimeyasoma na kuyaelewa maelekezo yote ambayo ni pamoja na sheria na kanuni za shule na nimekubali kuingia kidato cha tano katika shule ya sekondari Nyakahura kuanzia tarehe…………………….hadi nitakapo maliza kidato cha sita.

(b) Kwa hiyo naahidi kwamba:-

I. Nitazitii sheria zote za shule na kutimiza mambo yote muhimu yaliyotajwa
II. Sitashiriki vitendo vya hujuma wala vitendo ambavyo vitakuwa kinyume na uongozi wa serikali ya Jamhuri ya muungano wa Tanzania.
III. Nitatunza mali ya umma ambayo ni pamoja na majengo, samani, vitabu n.k.

Tarehe …………………….…………………sahihi ya mwanafunzi……........……

**<u>AHADI YA MZAZI/MLEZI</u>**

Mimi …………………………………….. ambye ni mzazi/mlezi wa mwanafunzi……………………………………………….. ninahaidi kwamba:-

1. Nitashirikiana na uongozi wa shule, walimu na watumishi wasio walimu katika kuhakikisha, mwanangu anatii sheria na kanuni za shule ya sekondari Nyakahura na iwapo atashindwa kutii sheria hizo, nitalazimika kukubaliana na uamuzi utakaofanywa na uongozi wa shule.

2. Nitafanya kila niwezalo kumwezesha mwanangu, kusoma kwa kulipa michango yote kama ilivyoelekezwa na shule.

Tarehe………………

Sahihi………………………Namba ya simu:………………..………………

# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA


SHULE YA SEKONDARI NYAKAHURA,
S.L.P. 193,
BIHARAMULO.

**MGANGA MKUU WA MKOA/ WILAYA/KITUO CHA AFYA**

JINA (mwanafunzi) ……………………… amechaguliwa kujiunga na kidato cha ……….…………….katika shule hii, ili kuendelea na masomo ni lazima apimwe kwanza. Nitafurahi iwapo mbali na kupimwa kijana huyu ataangaliwa uwezo wa kuona macho yake. Kama imeshauriwa avae miwani hana budi kuinunua yeye mwenyewe kwa fedha yake . Tafadhari nijazie sehemu inayohusika chini baada ya kupima.

Ahsante kwa ushirikiano

Wako katika kazi



BRAISON UHAKULA
MKUU WA SHULE




Nimempima mwanafunzi aliyetajwa hapo juu nakuona kwamba ana /hana matatizo/ugonjwa wa;

A. Kifua kikuu…………………………………………………………
B. Macho………………………..……………………………………
C. Masikio…………………………..……………………………
D. Akili……………………………………………………………………
E. Kilema chochote ……………………………………………………
F. Choo…………………………………………………………………………
G. Kwa wasichana tu nimeona ana/hana mimba ……………………… (***tafadhari usijaze bila kupima kipengele hiki)***
H. Athma…………………………………………………………………
I. Mengineyo……………………..………………………………………
J. Maoniya mganga …...........................................................................

SAINI NA MHURI WA OFISI……………………………
……………………………………………………………
MGANGA MKUU WA MKOA/WILAYA/KITUO CHA AFYA ………………
…………………………….
TAREHE …………………………..…………………………………………………